

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

**Fomu Maalum ya Kujaza Alama za Mwanafunzi katika
Upimaji wa Kusoma**

Jina la Mwanafunzi _____

Namba ya Mwanafunzi _____

Jina la Shule _____

Wilaya _____

Mkoa _____

KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU		
Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mpimaji
1.		
2.		
3.		
Jumla		

1. Kusoma maneno (alama 12^{1/2})

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia (**Ø**) neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi alama **00^{1/2}**)

televisheni	gita	vitamini	Wiki	Picha
kompyuta	pini	mdomo	sentensi	nyumba
tochi	baiskeli	mwanafunzi	ubao	mwavuli
chumvi	saa	mbwa	mwezi	kikombe
mchele	mkono	mwanga	karoti	jogoo

Alama:

2. Kusoma sentensi (alama 25)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (**Ø**) neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 1**)

Mbuzi wangu wana mikia mifupi.

Njoo hapa dada yangu mpole.

Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.

Viatu vyangu vyote ni vyeusi.

Hawa ni watoto wadogo sana.

Alama:

3. Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (**alama 12¹/₂**).

Sikiliza kwa makini wakati mwanafunzi anasoma kifungu cha maneno. Baada ya mwanafunzi kusoma,

chukua karatasi aliyokuwa anasoma kisha muulize maswali yaliyopo chini ya kifungu cha maneno.

Furaha ana umri wa miaka nane. Anaishi Kinondoni na kaka yake mkubwa. Mara zote hutunza vitu vyake vizuri. Siku ya Jumatatu, Furaha alikwenda dukani kununua Penseli. Alikuwa na shilingi mia tano mfukoni. Alinunua penseli mbili kwa shilingi mia nne. Furaha alibaki na shilingi mia moja ambazo alizitumia kununua kifutio.

Maswali na Majibu

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengele (d) alama $3\frac{1}{2}$, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo:

Na	Maswali na majibu	alama	
(a)	Furaha ana umri wa miaka mingapi? (nane)	3	0
(b)	Furaha anaishi na nani? (kaka yake mkubwa)	3	0
(c)	Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? (dukani)	3	0
(d)	Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? (alinunulia penseli mbili na kifutio)	3 ¹ / ₂	0
	Jumla ya alama		